**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UCHUKUZI**

# MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

**Tarehe:** 26 Agosti, 2024

**Mahala:** Viwanja vya Jamhuri - DODOMA

---

**Mhe. Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mgeni Rasmi kwa Hafla ya Uzinduzi ya Wiki ya Usalama Barabarani.**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(a) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, pamoja na mambo mengine, Mamlaka ina wajibu wa kuhamasisha ushindani wenye ufanisi miongoni mwa watoa huduma zinazodhibitiwa. Katika kutekeleza sehemu ya wajibu huo, Mamlaka iliandaa Tuzo za Wasafirishaji Bora na Salama kwa huduma zilizotolewa kwa mwaka 2023/2024 kupitia mabasi yaendayo mikoani na Nchi jirani.

Lengo la kuanzisha tuzo hizi ni kutambua mchango wa wadau wetu na pia kujenga hamasa ya wao kwa wao kushindana katika kuboresha huduma, kutangaza ubora wa huduma, kupata wateja/abiria zaidi ya waliokosa tuzo na hivyo kuwafanya waliokosa tuzo wajitahidi kuboresha pia nao waje wapate tuzo. Kwa ujumla ni kutambua, kuthamini na kuonesha shukrani kwa wadau wetu. Tumeanza na maeneo machache, miaka ijayo tutaendelea kuboresha na kuenda katika maeneo hata ya kutambu madereva bora na mahiri, makondakta bora na mahiri n.k. Aidha, tutakwenda pia upande wa Reli.

## (1) Tuzo ya Wasafirishaji Bora na Salama – Usafiri wa Mabasi ya Mikoani na Nchi Jirani

Mamlaka ilikasimisha kazi hii kwa Kamati Maalum iliyohusisha wataalamu kutoka taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na **Jeshi la Polisi - Kikosi cha Usalama Barabarani, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Chuo cha Ufundi Stadi (VETA), Mabalozi wa Usalama Barabarani (RSA), Taasisi ya Usafirishaji na Lojistik (CILT-Tanzania), Baraza la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na LATRA (LATRA CCC) na Wakala wa Barabara (TANROADS).**

**(2) Tuzo ya Vyama vya Wasafirishaji – Usafiri wa Mabasi na Magari ya Mizigo**

Aidha, Katika shughuli zetu tuna wadau ambao wametupa ushirikiano mkubwa katika kipindi cha mwaka 2023/2024 na kwa kutambua mchango wao katika kuboresha huduma za usafiri ardhi, tumeamua kuwa TUZO ya LATRA kwa mwaka 2023/2024.

**(3) Tuzo Maalum kwa Ushirika wa Waendesha Pikipiki – Usafiri wa Kukodi**

Kanuni za LATRA za Usafiri wa Magari ya Kukodi, 2020 ilifanyiwa marekebishwa Machi, 2023 na kuruhusu LATRA kukasimu madaraka ya kutoa leseni kwa Wakala Aliyethibitishwa (Authorized Agents) – Ambao ni  Vyama Ushirika, Taasisi za Umma (LGA), Kampuni, Watu Binafsi.

LATRA inatoa kipao mbele kwa SACCOS za Pikipiki kwa kuwa kupitia SACCOS hizi, vijana watajiajiri watapata asilimia 20 ya mapato ya leseni zote watakazotoa na watadhibitiana wenyewe kwa wenyewe (self-regulation). Hii itasaidia kutambuana kwenye vituo, kuepusha wizi na ujambazi, pia kuboresha huduma na usalama wa abiria.

Chama cha Kwanza cha Ushirika **Kilimanjaro Bajaji and BodaBoda Savings and Credit Cooperative Society (KOBABOT SACCOS LTD) ilisajiliwa 3 Agosti 2023**.

Kwa sasa Wanatoa Leseni za LATRA kwa Pikipiki kutumia Mfumo wa LATRA wa kutoa leseni (RRIMS) na wamepata fursa ya kuaminiwa na Taasisi zingine za umma na kupewa kazi zinazowaingizia mapato, mfano:kusimamia huduma za uegeshaji magari (parking).

Katika mafanikio haya ya KIBABOT SACCOS Ltd, naomba nimshukuru sana na kumpongeza sana Mhe. Nurdin Babu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, kwa namna alivyolisimamia suala hili yeye binafsi, na pia kwa kushirikiana na viongozi wa vyama vya siasa mkoani humo.

Nitumie fursa hii kutoa wito kwa SACCOS nyingine za Pikipiki, waige mfano wa KIBABOT SACCOS Ltd, wajipange tuwape mafunzo na waanze kutoa leseni za LATRA. Kwa

kufanya kazi hii, LATRA inawarejeshea mapato ya asilimia 20 kwa kila leseni, yaani kwa kila Shilingi 10,000/-, tunarejesha Shilingi 2,000/- na Mfumo wa RRIMS unautumia bure.

**WASHINDI NA TUZO ZA LATRA KWA MWAKA 2023/24**

Naomba sasa, kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa LATRA, niwataje washindi watatu katika kila kundi (wadogo, wakati na wakubwa) ili uwakabidhi Tuzo ya LATRA zao.

**Washindi wa tuzo za mtoa huduma za usafiri bora na salama kwa mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani – wenye mabasi 3 hadi 10**

**3. RATCO EXPRESS**
**2. ACHIMWENE BUSINESS GROUP LTD**
**1. SAMA LUXURY COACH**

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi,***

**Washindi wa tuzo za mtoa huduma za usafiri bora na salama kwa mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani – wenye mabasi 11 hadi 30**

**3. NGASERE CO. LTD**
**2. SATCO EXPRESS**
**1. TILISHO CO. LTD**

**Washindi wa tuzo za mtoa huduma za usafiri bora na salama kwa mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani – wenye mabasi zaidi ya 30**

**3. ABC UPPER CLASS LTD**
**2. HAPPY NATION CO. LTD**
**1. SHABIBY LINE**

**Pia naomba ukabidhi tuzo ya MSHINDI WA JUMLA miongoni mwa makundi yote matatu (wakubwa, wakati na wadogo), ambaye ni TILISHO CO. LTD**

Aidha, Tunaomba ukabidhi vyeti vya utambuzi kwa Vyama vya Wasafirishaji ambao wamekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa kazi za Mamlaka kwa mwaka 2023/24 kama ifuatavyo:

(i) Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA);
(ii) Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania (TATOA);
(iii) Chama cha Wamiliki wa Malori Wadogo na Wakati Tanzania (TAMSTOA);
(iv) Chama cha Wasafirishaji Tanzania (TAT); na
(v) Chama cha Wasafirishaji Mizigo kwa Njia ya Barabara Tanzania (TRFA).

Na kiupekee kabisa, Chama cha Ushirika na Mikopo cha Watoa Huduma za Bajaji za Abiria na Bodaboda Mkoani Kilimanjaro (KIBABOT SACCOS) ambacho ni chama cha kwanza kutoa leseni za pikipiki na bajaji kwa wanachama wao.

CPA Habibu J. Suluo

**MKURUGENZI MKUU - LATRA**